

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na: MTC/I.20/2/153

17/05/2021.

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

NAFASI YA AJIRA YA KADA YA MTENDAJI WA KIJINI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Makambako, anapenda kuwatangazia watanzania wote wenye sifa, kuomba nafasi wazi ya Ajira ya Mtendaji wa Kijiji nafasi tano (5) katika masharti ya kudumu.

AFISA MTENDAJI WA KIJINI DARAJA LA III: NAFASI 5 (VILLAGE EXECUTIVE OFFICER III)

SIFA ZA MWOMBADI:

1. Awe na elimu ya kidato cha nne au sita.
2. Awe amehitimu mafunzo ya Astashahada/cheti (NTA level 5) katika moja ya fani zifuatazo:-
Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.
3. Awe na umri usiozidi miaka 45.

KAZI NA MAJUKUMU:

- (i) Afisa Masuuli na Mtendaji wa Serikali ya Kijiji.
- (ii) Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao kuwa mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala bora katika Kijiji.
- (iii) Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- (iv) Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- (v) Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- (vi) Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na

- kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati kama vile kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- (vii) Kiongozi wa Wakuu wa vitengo vya kitaalam katika kijiji.
 - (viii) Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
 - (ix) Mwenyekiti wa kikao cha wataalam waliopo katika kijiji.
 - (x) Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za kijiji.
 - (xi) Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wannchi.
 - (xii) Atawajibika kwa Afisa Mtendaji wa Kata.

NGAZI YA MSHAHARA:

TGS B1, Tshs.390, 000/= kwa mwezi.

MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBALI WOTE AMBAYO NI YA LAZIMA KUZINGATIWA:

- 1. Mwombaji ni lazima awe ni raia wa Tanzania.
- 2. Awe hajawahi kufungwa kwa makosa ya jinai.
- 3. Awe hajawahi kupunguzwa/kufukuzwa kazi Serikalini.
- 4. Maombi ni lazima yaambatanishwe na vivuli vya vyeti vya kuzaliwa, kuhitimu Elimu ya Sekondari na vyuo vya mafunzo/taaluma.
- 5. Awe na Umri usiozidi miaka 45.
- 6. Maombi lazima yaambatanishwe na picha 2 za Passport size za hivi karibuni(ziandikwe majina kwa nyuma).
- 8. Maombi lazima yaambatanishwe na Wasifu binafsi (CV) zenyewe wadhamini wawili na mawasiliano ya uhakika, Anuani, barua pepe na namba za simu.
- 9. Awe hajaajiriwa wala hajawahi kuajiriwa Serikalini.
- 10. Awe na umri wa zaidi ya miaka 18.
- 11. Hati za matokeo za kidato cha nne, kidato cha sita na za vyeti vya Taaluma hazitapokelewa
- 12. Watumishi wa Umma walioajiriwa wahakikishe wanapitisha maombi yao kwa Waajiri wao
- 13. Watakaoitwa kwenye usaili watajigharamia wenywewe
- 14. Maombi yanaweza kuandikwa kwa kutumia lugha ya Kiswahili au Kiingereza
- 14. **Awe tayari kufanya kazi eneo lolote atakalopangiwa ndani ya Halmashauri ya Mji Makambako.**

MAOMBI YOTE YATUMWE KWENYE ANUANI IFUATAYO:-

MKURUGENZI,
HALMASHAURI YA MJI,
S.L.P 405,
MAKAMBAKO.

MWISHO WA KUTUMA MAOMBI NI TAREHE 30/05/2021

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:



**Paulo S. Malala
MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI
MAKAMBAKO.**

**MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI
MAKAMBAKO**

Halmashauri ya Mji Makambako, Mtaa wa Sigrid, Barabara kuu ya Njombe, S.L.P 405 Makambako, Njombe, Nukushi Na:
026-2968891, Simu Na: 026-2968892,
Barua Pepe: td@makambakotc.go.tz, Tovuti: www.makambakotc.go.tz